# Mikakati ya Kudumisha Hejemonia katika Siasa na Uchumi: Mfano wa Riwaya za *Dharau ya Ini*, *Msimu wa Vipepeo*, *Msururu wa Usaliti* na *Majilio ya Mkombozi*

*Harrison Onyango Ogutu, Wendo Nabea* na *Sheila P. Wandera-Simwa*
*Chuo Kikuu cha Laikipia*

**Ikisiri**

**Makala haya yanaangazia suala mikakati ya udumishaji wa hejemonia katika siasa na uchumi kama inavyodhihirika katika riwaya teule za Kiswahili. Makala haya yanachunguza ufanifu wa mikakati inayotumiwa na mabwanyenye kuendeleza na kudumisha hejemonia mintarafu ya riwaya za *Msimu wa Vipepeo, Dharau ya Ini, Msururu wa Usaliti* na *Majilio ya Mkombozi.* Mihimili ya nadharia ya hejemonia inayofafanua jinsi watawala hudumisha utawala wao kwa kutumia mikakati mbalimbali ilitumika katika kuhakiki data. Aidha makala haya yanatoa hamasisho kwa wanajamii kuhusu mikakati inayotumiwa na viongozi kuwashawishi raia waendelee kuunga mkono utawala uliopo hususan katika hali ambapo kihalisia wanafaa kuukosoa na kuupinga.**

**Maneno ya Kimsingi**: hejemonia, mahejemoni, mikakati ya kudumisha hejemonia, safu ya hejemonia

## Utangulizi

Makala hya yanajadili hejemonia kama hali ambapo watu walio na uwezo na mamlaka fulani huwadhibiti na kuwatawala wengine kwa ushawishi na ugagamizi. Watu hawa wenye uwezo na mamlaka ndio wanarejelewa kama mahejemoni katika makala haya. Mikakati ya kuendeleza na kudumisha hejemonia ni mbinu ambazo mabepari na mabwanyenye wanatumia kufanikisha utawala juu ya raia. Mbinu hizi zinawasaidia mabepari na mabwanyenye kuwapumbaza raia waridhie na kuidhinisha hejemonia. Matumizi ya mikakati hii inawafumba raia macho hivi kwamba wanaendelea kuunga mkono utawala uliopo licha ya manufaa madogo wanayopata. Mabwanyenye wanafanikisha uongozi wao wa kihejemonia juu ya watawaliwa kwa kuwashawishi waridhike na mawazo na hali iliopo. Kwa kuamini na kusadiki uongozi uliopo, raia wanaridhia yote wanayoambiwa na viongozi wao. Baadhi ya raia hawajali wala kutathmini madhara ya uongozi wa kihejemonia ilmradi wananufaika angaa kwa kiwango kidogo.

Maridhiano kati ya mahejemoni na watawaliwa hata hivyo yanaafikiwa kwa kutumia mbinu namna kwa namna ili kuwashawishi watawaliwa wakubali mawazo,

dhana na itikadi za uongozi uliopo. Katika hali ya kawaida raia wanatarajiwa kukosoa na kupinga unyonyaji na dhuluma zinazoendelezwa kupitia hejemonia. Hili haliwi rahisi kwa sababu asilimia kubwa ya raia wanapumbazwa kwa vishawishi anuwai. Baadhi ya mikakati inayotumiwa na mahejemoni kuwashawishi raia waridhie na kuidhinisha hejemonia ni kama vile: sheria, vyombo vya habari, vyombo vya dola, uchochezi na makongamano.

## Msingi wa Kinadharia

Nadharia ya hejemonia ilioasisiwa na Antonio Gramsci (1891-1937) imetumika katika makala haya. Makala yalijiegemeza kwenye mihimili ifuatayo ya hejemonia. Kwanza, ushirikiano na mwafaka kati ya watawala na watawaliwa. Kwa mujibu wa Fontana (2008) na Gramsci (1978), mfumo wa hejemonia unatokana na ushirikiano na muungano wa kimpango kati ya wafanyakazi na wakulima wadogo wadogo. Hivyo, makala haya yanaonyesha namna hejemonia inadumishwa na viongozi kwa maridhiano na mwafaka unaofungamanisha jamii ya kisiasa na jamii ya raia. Pili, uwezo wa kiuchumi ni muhimu katika ukuzaji na udumishaji wa hejemonia. Maoni ya Forgacs (1988) kuwa hejemonia sio suala la kijamii na kiitikadi tu bali pia huwakilisha uwezo wa kiuchumi yalisaidia makala haya. Makala haya hivyo basi yanaonyesha jinsi mahejemoni wanafanya jitihada zote kujitajirisha ili kwamba utajiri huo hatimaye utumiwe kuwashawishi watawaliwa. Raia wanaoishi maisha ya uchochole wanashawishika kwa wepesi kuingia makubaliano na viongozi wakwasi kwa kumegewa makombo ya mali inayomilikiwa na mahejemoni.

Nguzo ya tatu ni utamaduni wa jamii. Mintarafu ya mawazo ya Fontana (1993) na Boggs (1976), hejemonia inaelezwa na kuenezwa kupitia mfumo wa utamaduni wa jamii. Katika makala haya, mahejemoni hukuza na kudumisha hejemonia kwa kusisitiza haja ya kuzingatia mila na desturi za jamii. Kwa hivyo, makala yanadhihirisha namna utamaduni wa jamii hutumiwa kwa werevu kama njia ya kufikia masikizano baina ya mahejemoni na watawaliwa.

Nguzo ya nne ni mfungano baina ya hejemonia na udikteta. Mintarafu ya mawazo ya Ives (2004), Lenin (2004), Ransome (1992) na Gerratana (1975), ukosefu wa mwafaka kati ya mambo haya mawili huishia kwa viongozi kutumia nguvu. Makala haya yamemulika jinsi mahejemoni wanashinda upinzani sio kwa kutumia nguvu tu bali pia kwa kuungwa mkono kwa hiari na watawaliwa kupitia ushirikiano, kushirikishwa na masikilizano.

Hatimaye, Femia (1975) na Gramsci (1995) wanasisitiza wajibu wa wataalamu katika jamii yenye hejemonia pale ambapo mawazo na itikadi za mahejemoni hupitishwa hadi kwa watawaliwa kupitia wataalamu kama vile walimu, wanahabari, wanaharakati wa kisiasa na viongozi wa dini.. Makala haya yameangazia jinsi wataalamu wanachangia kuwepo na kudumu kwa hejemonia katika jamii wanapohusishwa katika masuala ya uchumi, siasa na utamaduni.

## Mikakati ya Kudumisha Hejemonia katika Siasa na Uchumi

### *Fadhila*

Viongozi wanatumia pesa na zawadi kama fadhila za kushawishi raia wakubali na kuidhinisha hejemonia. Kwa mfano katika *Msururu wa Usaliti*, mheshimiwa Mbogo anatumia utajiri wake wa kifedha kuwalaghai na kuwadhibiti kimapenzi wanawake vimada. Mbogo anawakodishia nyumba katika mitaa mbalimbali ya mji mkuu huku akiwakimu kikamilifu. Vimada hawa kwa kuleweshwa na wingi wa pesa wanazopewa, wanamsifu Mbogo kwa ukarimu wake na kufanya juu chini kudumisha uhusiano wa kimapenzi naye. Mabwanyenye wanawabadilisha wanawake wapendavyo na kuwatumia watakavyo na kisha kuwaacha ilmradi wanawake wenyewe wameridhia. Kwa mabwanyenye, wanawake ni kama muwa unaotafunwa na kufyonzwa maji tamu na kisha kutupa ganda maana halina kivuno tena. Mahejemoni wanawachezea wanawake kama wanasesere ambao wakishawapa raha na furaha wanayotaka wanaishia kuwagandamiza kwa kuwatupilia mbali. Suala kuu hapa ni kwamba, wanawake wanaoendelea kuwategemea wanaume kwa misaada ya pesa wanachangia uwepo wa utegemezi ambao unachochea kunawiri kwa hejemonia.

Kwa mujibu wa Fineman (2001), utegemezi unazidisha uovu kama vile upotovu wa maadili anaoshuhudiwa baina ya mabwanyenye na wanawake vimada. Wanaume wanawadhibiti na kuwatawala wanawake kwa kuwafanya wawategemee kiuchumi. Utegemezi wa misaada kutoka kwa wanaume miongoni mwa wanawake vimada ni hali inayothibitisha maoni ya Lautze na Hammock (1996) wanapodai kuwa utegemezi ni hali ya kutegemea rasilimali sana kiasi cha kutojidhibiti. Maridhiano baina ya wanawake na mabwanyenye yanachangiwa pakubwa na hali duni ya kiuchumi miongoni mwa wanawake wengi. Hali hii inawafanya wanawake wengi wasio na uwezo wa kujikimu kuwa mstari wa mbele kutetea hejemonia inayokuzwa na wanaume wenye uwezo wa kiuchumi. Hapa hejemonia inafaulu sana kutegemea uwezo wa kiuchumi wa mabepari na mabwanyenye kama inavyodai Forgacs (1988). Baadhi ya wanawake kwa hivyo wanaishi kwa kutegemea misaada ya pesa na mali kutoka kwa wanaume ambao wanawatumia wanawake hao kama vyombo vya mapenzi tu kisha kuwatupilia mbali wakishatimiza tamaa zao.

Mabwanyenye kama vile Rais wa nchi na Mheshimiwa Mbogo katika *Msururu wa Usaliti* wanatafuta ridhaa ya raia kwa kutumia pesa. Mabwenyenye wanatumia uwezo wao wa kifedha kutoa michango ya pesa katika mikutano ya harambee. Kwa mfano, Mheshimiwa Mbogo anahudhuria mikutano yote ya harambee inayofanywa na Rais wa nchi. Kwa sababu ni kama mwiko kutoa kiwango kikubwa cha pesa kuliko rais, Mbogo anahakikisha kuwa kiwango chake cha mchango kinakuwa cha pili kwa Rais. Ili kuungwa mkono na raia, Mbogo anajitapa kifua kwa kuzungumzia sana ukubwa wa michango yake kila anapowahutubia raia. Hii ni mbinu faafu ya kuwashawishi wananchi kuwa mahejemoni ni viongozi wanaopenda maendeleo. Kwa njia hii, wengi wa raia wanaridhia na kuidhinisha hejemonia bila pingamizi

hata kama mfumo wenyewe wa uongozi una kasoro chungu nzima. Mwandishi wa *Msururu wa Usaliti* anasema:

> Sasa harambee ilikuwa ni kama mashindano ya utajiri. Matajiri walitoa mabunda ya manoti kujionyesha kama warembo wajionyeshavyo katika shoo za fasheni. Harambee pia ilikuwa imegeuka na kuwa silaha ya kisiasa. Silaha iliyotumiwa na magwiji wa siasa za enzi hii kujidumisha madarakani na kuwaponda maadui wao… (uk 43).

Mabwanyenye wanatumia pesa kutoa michango mikubwa mikubwa kwa katika mikutano ya harambee. Kuhudhuria mikutano ya harambee na kutoa pesa hadharani ni njia nzuri ya kujionyesha kwa raia ili wamuunge mkono bepari anayetawala. Wanafanya hivi kwa madai ya kusaidia miradi mbalimbali katika jamii ilhali wanatumia njia hii kutafuta ridhaa ya raia. Michango ya harambee ni moja ya njia zinazotumiwa na mabwanyenye kujidumisha mamlakani huku wakiwabeza wakosoaji wa hejemonia wasio na uwezo wa kiuchumi. Raia wanaokubali kushawishika kwa njia hii ya kupewa pesa wanarutubisha kukua na kunawiri kwa hejemonia katika jamii.

Wawaniaji wa nyadhifa za uongozi wasio na uwezo wa kiuchumi wanashindwa katika kinyang'anyiro cha uongozi kwa kukosa pesa. Kwa mfano, katika *Msururu wa Usaliti* mwanasheria tajika (Nkando) wa kutetea haki za wanawake na mpinzani wa Mheshimiwa Mbogo anaporomoshwa na Mbogo katika kinyang'anyiro cha uchaguzi kwa kukosa pesa za kuhonga wapiga kura. Mbogo anaitisha mikutano mitano ya harambee katika sehemu mbali mbali za eneobunge lake wakati wa kampeni za uchaguzi. Miwili kati ya mikutano hiyo, ni ya kuchanga pesa za kujenga makanisa. Mkutano mwingine ni wa kusaidia makundi ya kina mama na mwingine wa kuanzisha mfuko wa kuwasaidia watoto werevu wanaoshindwa kulipa karo za shule na hatimaye ule wa kujenga josho la mifugo. Kwa uwezo wake wa kifedha, Mbogo anatembea mchana kutwa kutoka nyumba hadi nyingine akiwashawishi raia kwa maneno matamu na zawadi kama vile sukari, pakiti ya sembe au shilingi chache. Kwa kutumia mbinu hii, bwanyenye huyu anachaguliwa kuendeleza utawala wake juu raia licha ya kuwa hana sifa za kiongozi bora. Mahejemoni wanaojali maslahi yao tu huku wakiwagandamiza raia kwa kuwapumbaza na zawadi ndogo ndogo wakati wa uchaguzi, wanadumu mamlakani kwa ridhaa na idhini ya raia wanaowachagua. Wanatumia pesa kugeuza uongo kuonekana kama ukweli, chuki kuonekana kama mapenzi, huzuni kuonekana kama furaha. Raia wanaoridhia vishawishi vya namna hii wanawasaidia mahejemoni kusalia mamlakani kwa muda mrefu. Watawang'oaje madarakani ilhali wanapokezwa zawadi na pesa kutokana na mwafaka uliopo wa kukuza hejemonia?

Katika malezi ya watoto, baadhi ya wazazi wanaoendeleza na kudumisha hejemonia wanatumia zawadi na pesa kuwashawishi watoto waridhie mawazo yao. Kwanza, katika *Msururu wa Usaliti* Mheshimiwa Mbogo akiwa mzazi wa Kage ni bwanyenye anayetumia uwezo wake wa kifedha kumshawishi bintiye akubaliane

naye. Akitoa ahadi kwa Kage, Mbogo anasema anasema: "Nataka kutumia uhusiano wangu na watu wazito kukupatia kazi ya maana. Nangoja tu uniambie kazi unayoitaka. Chaguo ni lako... ukitaka naweza kukuchagulia," (uk 29). Pili, katika *Msimu wa Vipepeo*, Waziri Mkurutu anaendeleza na kudumisha hejemonia ya kijamii katika familia yake kwa kutumia mali na utajiri wake. Akimtaka bintiye wa kambo (Ndumi) aridhie mawazo yake kama mzazi, waziri anaamuru Ndumi awe akipelekwa shuleni na kuchukuliwa shuleni kwa gari kubwa la waziri. Zaidi, waziri anamnunulia Ndumi simu ya mkononi ya kipekee yenye kamera na uwezo wa kuhifadhi picha za video. Ushawishi na ugagamizi unaofanywa kwa kutumia pesa na zawadi unafaulisha hejemonia. Baadhi ya wazazi wanawatawala na kuwadhibiti watoto wao kwa kutumia uwezo wao wa kiuchumi. Hivyo, wanatumia uwezo wao wa kifedha na mali kushawishi watoto waridhie hejemonia inayokuzwa na kudumishwa katika familia. Wanafanya hivi kwa kuwapa watoto wao zawadi kama njia ya kuwabembeleza wakubaliane na kuidhinisha mawazo na dhana zao. Wazazi wanakuwa mahejemoni wanaowataka watoto waridhie hali iliyopo kwa kuwapendekezea na kuwawasilishia mawazo ambayo ni vigumu sana kuyakosoa au kuyapinga. Mawazo kama vile kutafutiwa ajira baada ya kuhitimu kutoka chuo kikuu katika jamii ambayo nafasi za ajira zimeadimika sana yanalenga kushawishi na kugagamiza watoto ili waridhie hejemonia.

Mabwanyenye wanatumia pesa kuandaa karamu za kukata na shoka kuwashawishi raia waridhie utawala wao. Mathalani, Munene katika *Dharau ya Ini* anapofanya maandalizi yake ya kugombea nafasi ya uenyekiti wa chama, anaandaa karamu kuwafurahisha wafuasi wake (uk 101). Pia, Rais (Mzee), katika *Msururu wa Usaliti*, anaandaa ikuluni sherehe ya karamu za vinywaji na vitafunio kuwakaribisha wanasiasa wanaoasi upinzani. Mabepari wanawastarehesha raia kwa kuwaandalia karamu spesheli kama njia ya kuwafumba macho wakubali utawala. Mahejemoni hutumia fursa hizi kuuza sera na mawazo yao kwa wafuasi. Karamu kama hizi zinanuia kuyeyusha mioyo ya wafuasi ili waridhie na kuidhinisha hejemonia. Mahejemoni mara nyingi wanatumia utajiri wao kutafuta uungwaji mkono katika utawala kwa kuwahonga na kuwanunua maskini ili wawasaidie kuafikia matamanio yao. Karamu za vyakula na pesa kidogo kwa watu maskini ni vishawishi mwafaka kwa raia ili wapige jeki udumishaji wa hejemonia katika jamii. Raia wenye njaa na tamaa ya pesa wanaishia kuwa vikaragosi na mawakala wa kukuza na kuendeleza hejemonia.

Uwezo wa kifedha na mali alionao waziri Mkurutu katika *Msimu wa Vipepeo* unamwaminisha Julia mkewe kuwa huyu ndiye mume anayefaa zaidi ulimwenguni kote. Mkurutu anamiliki vifaa vya kisasa kama vile kitanda cha samadari, televisheni ya sony triton, mashine ya DVD, piano, makabati makubwa ya nguo, bafu la kisasa lenye bomba na legeni la kuogelea na godoro la maji. Vyote hivi na vingine vingi vinamridhisha na kumwaaminisha Julia, msichana wa watu aliyezaliwa na kulelewa katika mazingira ya uchochole kuwa Mkurutu ni mume bora sio gumegume. Baadhi ya wanawake katika ndoa wanaridhia hejemonia inayokuzwa na waume zao kwa kuruhusu mawazo na fikira za ufanisi wa waume

zao kuwatawala. Wanawake wa namna hii wanafumbwa macho na mali ya wanaume kiasi kwamba wanakosa kuona madhila yaliofichika katika hejemonia inayokuzwa na wanamume katika ndoa. Ukwasi wa baadhi ya wanaume katika ndoa unatumika kuwashawishi baadhi ya wanawake wakubali hejemonia inayodumishwa na wanaume kama hali ya kawaida. Watawaliwa (wanawake katika muktadha huu) wanasaidia kukua na kuendelea kwa hejemonia wanapokubali udhalimu wa mahejemoni (wanaume) ilimradi wanufaike kutokana na utajiri wa waume zao. Watawaliwa wanakosa sauti ya kukosoa madhila ya hejemonia kwa kuruhusu ufukara wao kuwa kigezo cha maamuzi. Wanawake wenye tamaa ya mali na utajiri wa haraka wanakuwa mawakala wazuri wa kuendeleza na kudumisha hejemonia inayokuzwa na wanaume katika ndoa.

***Vikwazo vya Kiuchumi***

Mataifa yaliyoendelea yanakuza na kuendeleza hejemonia juu ya mataifa machanga kiuchumi kwa namna yanavyotoa ufadhili. Mathalani, mwandishi wa *Msururu wa Usaliti* anasema: “Mbogo na wabunge wenzake walikuwa katika warsha ya siku tatu. Hii ilikuwa hatua mojawapo iliyochukuliwa na mataifa wafadhili kuishinikiza serikali kuimarisha demokrasia” (uk 26). Warsha hii inafanywa kwa madhumuni ya kupiga msasa katiba ili kufaulisha siasa ya vyama vingi mintarafu ya matakwa ya wafadhili. Nchi zenye uwezo mkubwa wa kiuchumi zinapumbaza nchi zenye chumi dhaifu kwa kuwapendekezea haja ya kukumbatia demokrasia kama mfumo bora wa utawala huku wakilenga kutumia udhaifu wa demokrasia kukuza hejemonia. Hali hii inadhihirika katika maoni ya Forgacs (1988) anaposema kuwa mahejemoni wanatumia uwezo wa kiuchumi kama msingi wa kushawishi watawaliwa. Viongozi wa nchi changa, wanaridhia matakwa ya wafadhili na kuandaa warsha na makogamano yenye madhumuni ya kuafikia mawazo na matamanio ya mahejemoni. Viongozi wa nchi changa wanakosa kuona hila za mataifa yalioendelea. Hivyo, wafadhili wanaendeleza utawala wao juu ya wafadhiliwa kwa kuwapendekezea mawazo na sera ambazo sio rahisi kupingwa.

Mashirika ya kifedha ulimwenguni hutumiwa na mataifa yalioendelea kutawala mataifa machanga. Kwa mfano, katika *Msururu wa Usaliti* na *Msimu wa Vipepeo* mataifa ya Ulaya na Marekani yanadhibiti mashirika ya kutoa mikopo kama vile Benki kuu ya Dunia na Mfuko wa Kifedha wa Kimataifa. Mashirika haya mawili hutumiwa na mataifa yalioendelea kiuchumi kama vile Marekani, Uchina na baadhi ya nchi za Uropa kutoa ufadhili kwa mataifa maskini yanayoridhia mawazo, sera na itikadi zao. Mashirika haya ya kifedha aidha yanatumika kama polisi wa kiuchumi kwa mataifa maskini. Hapa, mataifa machanga yanatiwa hofu iwapo hayataridhia matakwa ya wafadhili. Mataifa wafadhili yanakuwa mahejemoni wanaotumia vikwazo vya kiuchumi kuyashawishi mataifa machanga yaridhie hejemonia. Ufadhili na misaada mingine ya kifedha kwa nchi changa kiuchumi inategemea iwapo nchi zinazoendelea zinakubali mawazo, sera na itikadi za wafadhili. Sera, mawazo na itikadi za wafadhili zinawasilishwa kwa njia bembelezi kwa kuonyesha

raia wa nchi changa watakavyofaidika katika uhusiano mpya., Vikwazo vya kiuchumi kwa mataifa machanga ni njia mwafaka ya kuhakikisha kuwa hejemonia inaendelezwa na kudumishwa kwa makubaliano kati ya mahejemoni na watawaliwa. Kwa njia hii, viongozi wa mataifa machanga hawana budi ila kuridhia na kuidhinisha hejemonia kwa kutazamia manufaa yanayoambatana na mfumo huo. Hali kwamba mataifa machanga kiuchumi yanategemea misaada na ufadhili kutoka kwa mataifa yalioendelea inachangia pakubwa udumishaji wa hejemonia. Mwangwi wa mawazo haya unashuhudiwa katika maoni ya Lensink na White (1999) wanapodai kuwa taifa linakuwa tegemezi kwa misaada iwapo taifa hilo haliwezi kutimiza lengo fulani bila ya kupewa au kupata msaada kutoka nje. Kwa hivyo, vikwazo vya kiuchumi vinayafanya mataifa machanga kiumi kutegemea mataifa yalioendelea; hali ambayo inakuza na kudumisha hejemonia.

### *Sera ya Tenga-Tawala*

Viongozi wanawagawanya wanajamii kwa misingi ya vigezo vya kikabila ili kuwadhibiti na kuwatawala. Kwa mujibu wa *Msururu wa Usaliti,* uongozi wa Afrika baada ya uhuru, uliendelezwa kwa kutumia sera ya ukoloni. Viongozi walipiga sera ya tenga-tawala msasa na hatimaye ukoloni mamboleo ukawa mbaya zaidi kuliko Ukoloni mkongwe. Viongozi waliotwa hatamu za uongozi baada ya mkoloni kuondoka, wameishia kuwa watemi wa makabila yao badala ya kuwa viongozi wa taifa wanaojali na kushughulikia maslahi ya raia wanyonge. Viongozi wa Afrika baada ya uhuru wanakuza na kudumisha hejemonia kwa kutumia mbinu zilezile Wakoloni wakongwe walitumia. Viongozi wa Afrika wamekuwa mahejemoni wanaowatenganisha raia kwa kuwakabidhi zawadi ndogo ndogo na ahadi chungu nzima. Ahadi hizi zinawapa watawaliwa matumaini ya uongo kwamba maisha yatakuwa bora zaidi siku za usoni. Raia wanaokataa kuridhia mawazo na hila za viongozi hawa wanachukuliwa kuwa mahasimu ambao kamwe hawafai kutangamana na wale wanaokubaliana na hejemonia. Kwa njia hii, viongozi wanafaulu katika ajenda yao kwa kuvunja umoja ambao ungewapa watawaliwa nguvu za kupambana na hejemonia. Akirejelea sera ya tenga-tawala, mwandishi wa *Msururu wa Usaliti* anasema:

> Sera yao ya tenganisha-utawale iliyafanya makabila mbalimbali kuchukiana, kutuhumiana na kupigana... uongozi mpya wa Kiafrika ulijishughulisha na kuokota makombo yalioachwa na mkoloni. Kila mmoja alijiona kuwa mtemi wa kabila lake badala ya kiongozi wa kitaifa. Kazi ya kila mtemi ikawa ni kuwania kukata kipande kikubwa zaidi cha nyama kutoka kwa mzoga wa taifa. Ukataji ulifanywa kwa jina la kabila. Lakini ulipokamilika, mtemi alikula nyama pamoja na mke, watoto na jamii zake. Kabila lilitupiwa mifupa kupitia dirisha la kasri lake (uk 41).

Viongozi wa nchi za Afrika baada ya uhuru walirithi mfumo wa uongozi uliotumiwa na wakoloni wakongwe. Walirithi mbinu ya tenga-tawala na kuitumia kuwa watemi wanaotawala wananchi kwa kuwagawa kikabila. Viongozi hawa

wanafaulisha ajenda yao kwa kuwafitinisha raia dhidi ya raia wenzao kwa misingi ya kikabila. Ili kudumisha hejemonia, viongozi wanapiganisha kabila moja dhidi ya kabila lingine kwa kupanda mbegu za chuki. Makabila yanapopigana, raia wa kawaida ndio wanaoumia huku viongozi wakitafuta namna wanavyoweza kufaidika kutokana na vita hivi. Viongozi wanatumia fursa hii kuendeleza na kudumisha hejemonia kwa kujifanya kutafuta amani na upatanisho kati ya makabila yanayopigana. Wanaofaidika hapa ni viongozi wanaodumishwa mamlakani pamoja na familia zao. Mabwanyenye wanadumisha hejemonia kwa kuungwa mkono na watu wa makabila wanakotoka; watu ambao wameshawishika na kugagamizwa kwa kugawiwa makombo ya mali waliojilimbikizia mahejemoni hao.

***Sheria***

Sheria imetumiwa na mabepari na mabwanyenye kudumisha utawala na udhibiti juu ya raia. Artz na Murphy (2000) wanasema kuwa sheria ni mojawapo ya vipengele ambavyo sharti viambatane na mfumo wa kisiasa unaowakilisha haja na matamanio ya raia iwapo hejemonia itafaulu. Hivyo, mabwanyenye wanahakikisha kuwa sheria zinazotungwa zinawadumisha mamlakani bila ya watawaliwa kulalamika. Mathalani, katika *Msururu wa Usaliti*, mfumo wa chama kimoja cha kisiasa nchini ni sheria katika katiba ya nchi. Hivyo, Rais wa nchi anaishia kudumu madarakani kwa ridhaa na idhini ya raia. Sheria hii inamruhusu Mzee kugombea wadhifa wa urais mara nyingi atakavyo kwa makubaliano na raia. Ijapokuwa pawepo na wakosoaji wa sheria kama hii, viongozi wanafaulu kukuza hejemonia pasi ya pingamizi. Viongozi wanawashawishi na kuwapumbaza raia waridhie hejemonia huku wakidai kufuata sheria ya nchi. Viongozi, kwa kuelewa udhaifu wa watawaliwa wanahulutisha ufuataji wa sheria na uwezo wa kifedha kuwashawishi raia waridhie hejemonia. Watawaliwa wakishapumbazwa kwa hila kwamba viongozi hawajavunja sheria kwa kuwania tena na tena nyadhifa za uongozi, wanaishia kuwachagua mahejemoni wanaoendeleza hejemonia bila kupingwa.

Sheria inatumiwa na viongozi wa kisiasa kupiga vita wakosoaji wote wanaopinga utawala wao. Watumishi wa umma wanaokosoa viongozi wa kisiasa wanaotawala wanakumbana na vikwazo vingi vya kisheria. Katika *Msururu wa Usaliti* Dkt. Makau anayefanya kazi katika Hospitali Kuu ya Kitaifa anaachishwa kazi kwa misingi kwamba amevunja sheria kwa kujiunga na upinzani. Barua ya kuachishwa kwake kazi inasisitiza kuwa amevunja sheria inayowakataza wafanyakazi wa umma kushiriki siasa. Kwa hivyo, anaachishwa kazi ili kulinda maslahi ya umma (uk 109). Mfanyakazi wa umma yeyote anayejiunga au kushirikiana na wakosoaji wa serikali analaumiwa kwa kuvunja sheria inayowakataza kufanya hivyo. Sheria ambayo inamzuia mtumishi wa umma kuwa na uhusiano na wanaharakati wanaokosoa serikali ni gandamizi na yenye vitisho. Sheria kama hii inatumiwa na mahejemoni kugagamiza wafanyakazi wa umma ili wakubaliane na utawala wa kihejemoni uliopo. Viongozi wanafafanua sheria visivyo kuwapumbaza na kuwasadikisha watawaliwa kuwa watumishi wa umma

wanavunja sheria wanapokosoa au kuhusiana na wakosoaji wa hejemonia. Kwa mujibu wa sheria kama hizi, raia yeyote anayefanya kazi ya umma haruhusiwi kukosoa serikali kwa namna yoyote. Mfanyakazi yeyote wa umma anayekosoa uongozi wa kihejemonia uliopo anachukuliwa kuwa msaliti asiyependa nchi yake na mvunjaji wa sheria za nchi yake. Umma unafitinishwa dhidi ya raia kama huyo ili katu asiungwe mkono. Sheria, kwa hivyo ni chombo kinachotumiwa na mahejemoni kuwatia watawaliwa hofu watafakaripo adhabu kali inayoambatana na uvunjaji wa sheria iliopo. Kwa kufuata sheria kama hizi raia wanaishia kuridhia na kuidhinisha hejemonia.

Mabwanyenye wanatumia sheria katika kukuza na kuendeleza utawala wao kwa kuhusisha wanasheria wanaofasiri sheria visivyo. Mabwanyenye hutumia uwezo wao wa kiuchumi kuathiri utekelezaji wa sheria ili kujilinda na pia kulinda mali zao (Omboga, 1984). Katika *Dharau ya Ini*, mwanasheria Fabio Mkalla anateuliwa kuwa Mwanasheria Mkuu wa nchi; nafasi ambayo mabepari na mabwanyenye serikalini wanatumia vizuri kukuza na kuendeleza hejemonia. Kwa kuielewa sheria vizuri, Fabio anatumia mianya katika sheria kuwatetea na kufunika madhila ya mabwanyenye wenzake serikalini. Mathalani, anayakatiza mashtaka dhidi ya Gattuso Berlusconi (mwekezaji mwitaliano anayemuua kijana Yusuf Idris) kwa kutumia mamlaka ya kisheria ya ‘nolle prosecui’. Anadai kuwa hapana uchunguzi unaopelekea kushtakiwa kwa Gattuso Berlusconi na hata mashahidi waliokuwa tayari kuutoa ushahidi wao mahakamani wameghairi (uk 146). Mabepari na Mabwanyenye wanatumia mianya katika sheria za nchi kutetea kuwepo kwa hejemonia. Wapinzani na wakosoaji wa hejemonia wanakabiliwa kisheria kwa kunukuu vipengee vya sheria vinavyowapa mahejemoni haki na uwezo wa kutawala. Ofisi za kisheria nchini pia zinatumika kuwazima wakosoaji kwa kuwatia hofu ya kukumbana za ghadhabu za sheria iwapo watavunja sheria iliyopo. Mabwanyenye wanatumia sheria kiujanja kuzuia uwezekano wa yeyote kuthubutu kukabiliana na hejemonia inayokuzwa na kuendelezwa. Ushirikiano baina ya mabwanyenye na wanasheria ni njama wanayotumia kuhakikisha kuwa hejemonia inakua na kunawiri bila pingamizi. Mabepari wanawahusisha wanasheria wanaoelewa vipengee vidogo vidogo vya sheria na ambavyo havifahamiki na raia wengi ili kufaulisha azma yao ya kudumisha hejemonia. Nia ya mahejemoni ni kukuza na kuendeleza hejemonia kwa kupata uwezo wa kisiasa na kiuchumi unaowasaidia kujilimbikizia mali kwa ridhaa ya watawaliwa.

Kwa upande mwingine, kutokuwepo kwa sheria mwafaka za kuwahukumu watu wanaoshirikiana kutenda uovu ni rutuba kwa hejemonia. Kwa ufahamu kwamba hamna sheria inayowazuia mabwanyenye kutenda mambo fulani, utawala wao unadumishwa. Mathalani, katika *Majilio ya Mkombozi* Ilonkundemi anapotoka mafichoni na kukamatwa na polisi na kisha kuhojiwa juu ya mauaji ya ng’ombe wa Baikungi, anadanganya kuwa alikuwa pekee yake kwani hataki kumweka mjombake (Wapukorengonyi) matatani. Wanajamii na polisi wanajua kwamba hawa wawili walishirikiana kutekeleza uhalifu lakini kwa mujibu wa sheria hawana ushahidi. Kisheria, uhalifu wote ulitendwa na Ilonkundemi, kwa hivyo hukumu

itamhusu yeye pekee yake (uk 99). Ilonkundemi pekee ndiye anazuiliwa katika seli huku polisi wakiendelea kufanya mipango ya kumpeleka mahakamani. Ukosefu wa sheria ya kushika wapangaji wa uhalifu huku watekelezaji wakitiwa mbaroni na kufunguliwa mashtaka ni mwanya ambao mahejemoni wanatumia kwa ghiliba kudumisha hejemonia. Mabwanyenye wanapanga matendo ya uhalifu dhidi ya wapinzani na wakosoaji wao na kisha kuwatumia watu wengine hususan vijana wasio na ajira kutekeleza uhalifu huo. Uhalifu wenyewe unapangwa kwa nia ya kuwatia hofu wapinzani na wakosoaji wa hejemonia ili waridhie hali ilivyo. Watekelezaji wa uhalifu wanapatikana na hatia huku wapangaji wa uhalifu wenyewe wakiachiliwa huru. Mabwenyenye, kwa hivyo wanaendeleza hejemonia kwani hamna sheria inayoweza kuwashtaki iwapo watafanya uhalifu kupitia watu wengine.

***Vyombo vya Dola***

Vipengee vya kiutawala kama vile mahakama na polisi vinafungamanishwa na mfumo wa kihejemonia unaowakilisha matamanio ya raia (Artz na Murphy, 2000). Katika *Dharau ya Ini*, chifu Kivu na askari wanatumiwa na serikali ya ukoloni kuzima mgomo wa watu wanaodaiwa kuwazuia wafanyabiashara kusafirisha bidhaa zao. Ili kuwatia raia woga, Chifu Kivu anamgota kichwa mwandamanaji mmoja na kumchubua ngozi. Aidha, katika *Msururu wa Usaliti* vijana wa Chuo Kikuu cha CHUKI wanapogoma na kuandamana kupinga unyakuzi wa mali ya umma unaofanywa na viongozi mabwanyenye, wanatawanywa na kupigwa na polisi. Hali hii inathibitisha mawazo ya Nella (2017) anapodai kuwa hejemonia inahusu utawala wa kimawazo na pia utawala wa kimabavu ambapo mabwanyenye wanatawala na kudhibiti hali kwa kutumia nguvu za kijeshi. Polisi wanafanywa vikaragosi na mawakala wa kukuza hejemonia. Hawa wanapewa zawadi na mamlaka kuhakikisha kwamba hejemonia inanawiri kwa kuwatia hofu wakosoaji na wapinzani wa mfumo huu wa utawala. Kwa kutiwa woga na hofu, raia wanaishia kukubali matakwa ya viongozi hata kama kwa hali ya kawaida hawawezi kukubaliana nao. Viongozi wa kisiasa wanakuza uhusiano mzuri na polisi ili wawasaidie kuimarisha hejemonia katika jamii. Wapinzani wa hejemonia wanaonywa na kutiwa mbaroni na polisi kama njia ya kuwatia hofu ili wasitishe harakati zao za upinzani. Maoni haya yanaafikiana na mawazo ya Bate (1975) anayedai kuwa mahejemoni wanatumia mbinu za kisiasa na kijeshi kusitisha mawasiliano baina wanamapinduzi na wanaharakati wanaokosoa na kupinga hejemonia.

Katika *Dharau ya Ini,* polisi wanatumiwa kumnyamazisha King'o na kumtia adabu ili akubaliane na Munene. Baada ya King'o kupigana na Munene, polisi wanaingia kwake kwa ujeuri na dharau. Magurudumu ya gari la polisi yanakanyaga maharage. Polisi wanamwambia Wanza, mkewe King'o kuwa kila kitu; ardhi, kibanda chao na hata majani (maharage) anayolalamikia ni mali ya serikali na iko huru kuchukua wakati wowote (uk 95). King'o na Wanza wanakumbana na ghadhabu za vyombo vya dola ambavyo vinawatia hofu. Ili kuwatia wapinzani hofu

zaidi, vyombo vya dola vinatumia nguvu na vitisho kuwashawishi wapinzani waridhie matakwa ya hejemonia. Wakosoaji na wapinzani wanaonyeshwa na kusisitiziwa kuwa chochote wanachomiliki ni mali inayotokana na hejemonia wanayoipinga. Mawazo haya yanaoana na maoni ya Ives (2004), Lenin (2004), Ransome (1992) na Gerrattana (1975) wanaokubaliana kuwa watawaliwa wakikataa kukumbatia hejemonia inayokuzwa, mahejemoni huishia kutumia nguvu. Kulingana nao, matumizi ya shuruti na nguvu husaidia mahejemoni dhidi ya wapinzani wao. Hii ina maana kwamba hejemonia anakuzwa na kuendelezwa kwa misingi ya mfungamano wa mwafaka, masikilizano na udikteta. Hivyo, usalama wa wapinzani na wakosoaji wa hejemonia unategemea mlahaka mwema na mahejemoni wanaotawala. Kutokana na woga, baadhi ya wapinzani na wakosoaji wa hejemonia wanasalimu amri na kuidhinisha hejemonia kama mfumo bora wa utawala.

Serikali ya kihejemonia inahakikisha kuwa hali ya jela na korokoroni inakuwa mbaya zaidi kama njia ya kuwatisha raia ambao wanaweza kufikiria kuasi au kukaidi dhidi ya hejemonia. Kwa mfano, katika *Dharau ya Ini,* Wanza (Mkewe King'o) anapomtembelea mumewe jela anakatazwa na kuzuiwa kumwona. Chakula na ndizi anazobeba Wanza zinaishia mikononi mwa walinzi. Mkuu wa kituo amekataza yeyote au chochote kumfikia King'o. Hali ya King'o inasikitisha kando na kupewa kichapo cha mbwa mle korokoroni. Wakosoaji wa hejemonia hufungwa jela bila ya kesi zao kusikizwa na kuwekewa vikwazo vya kuzuia watu wa familia na marafiki kuwatembelea. Wafungwa wananyimwa mahitaji ya kimsingi kama njia kuwatia wakosoaji na wapinzani hofu. Isipokuwa pawepo na watu jasiri wanaoweza kukabiliana na mahejemoni wanaotumia vyombo vya dola, hejemonia inakua na kunawiri kwa kuwadhulumu wapinzani na wakosoaji. Kando na vyombo vya dola kuwatia hofu wapinzani, wakosoaji na raia kwa jumla, vyombo hivi visipodhibitiwa vinasababisha mateso yasiyomithilika. Hali hii ya mateso na dhuluma ndio inayowahofisha watawaliwa na kuwaacha bila chaguo ila kuridhia hejemonia. Mahejemoni wanatumia vyombo vya dola kuwashawishi raia kukubali na kuidhinisha utawala wa kihejemonia uliopo. Pingamizi ya aina yoyote dhidi ya hejemonia inakumbana na ukatili na dhuluma kubwa kutoka kwa vyombo vya dola.

Katika *Msimu wa Vipepeo,* mahakama zinatumiwa na mabwanyenye kutoa uamuzi na hukumu ambazo zinaunga mkono hejemonia. Kwa mfano, ndoa ya Melissa na mumewe inapovunjika baada ya miaka kumi na miwili ya dhiki na mateso, mahakama inamkabidhi mumewe haki ya kuishi na kuwatunza watoto. Katika jamii nyingi za kuumeni, kama ilivyo katika *Msimu wa Vipepeo* mamlaka, uwezo na utawala wanapewa wanaume. Kwa misingi hiyo, wanawake kama Melissa wananyimwa haki ya kulea watoto. Mahakama zinatumia sheria kukuza na kuendeleza hejemonia katika jamii ambapo wanaume aghalabu wanapewa mamlaka juu ya wanawake katika masuala ya ndoa na malezi ya watoto. Ufafanuzi wa sheria wenye upendeleo wa jinsia ya kiume unampa mwanamume utawala juu ya mkewe. Mahejemoni wanatumia mahakama kufafanua sheria visivyo na kisha kuhakikisha kuwa polisi wanatekeleza matakwa ya sheria hizo zilizofafanuliwa kwa upendeleo. Kwa njia hii raia wanashawishika kuridhia maamuzi ya vyombo vya dola; maamuzi

ambayo kimsingi yanatokana na ajenda ya mahejemoni inayomtaka mtawaliwa aridhie na kuidhinisha utawala uliopo. Vyombo vya dola vinatumika kudumisha hila na hadaa za uongozi wa kihejemonia kwa kuwatia watawaliwa hofu ili wasije wakakosoa wala kupinga sera za utawala.

Katika *Majilio ya Mkombozi,* sehemu za huduma muhimu kama vile visima, mito, misitu na malisho ya mifugo zinawekwa chini ya ulinzi wa majoka ya mchawi. Majoka haya ni taashira ya vyombo vya dola ambavyo vinatumika na mabepari na mabwanyenye kukuza na kudumisha hejemonia. Mwandishi akirejelea vishawishi na matakwa ya bwanyenye anayewakilishwa kwa taswira ya mchawi anasema:

> Asiyelipa kodi hiyo mpya hakuweza kupata huduma hizo muhimu. Watu waliodhubutu kuchota maji bila ya kufuata maagizo ya kodi, waliumwa na majoka wa mchawi. Wengine walikufa na wengine kuteseka kwa maisha magumu (uk 114).

Majoka hapa ni jazanda ya vyombo vya dola kama vile polisi wanaotumiwa na mabwanyenye kuwatia woga raia ili waridhie utawala. Raia wanakubali hali iliyopo kwa sababu wanashurutishwa kufanya hivyo. Raia wanatumia muda wao mwingi kujichumia ili waweze kulipa kodi na kuapuka gadhabu za vyombo vya dola. Mawazo haya yanaoana na maoni ya Strinati (1985) anapokaulisha kuwa, katika hali kama hii raia wanalazimika kutumia muda wao mwingi kujichumia huku wakiacha hali ya hejemonia iendelee jinsi ilivyo. Mabwanyenye wanatumia vyombo vya dola kuwatia watawaliwa hofu na kuwaogofya ili waidhinishe hejemonia. Vyombo vya dola vinatoa onyo na tahadhari kwa raia ambao hawakubaliani wala kuafikiana na utawala uliopo. Utoaji wa huduma muhimu unaachwa mikononi mwa mawakala wa mahejemoni ambao wanasisitiza kwamba raia waridhie matakwa fulani.

### *Miradi na Ahadi-Hewa*

Mabepari na mabwanyenye hutumia uzinduzi wa miradi kama njia ya kuwarai watawaliwa wakubali utawala. Katika *Msimu wa Vipepeo,* mradi wa ujenzi wa uwanja mkuu wa michezo mjini Kitambaasie pamoja na ujenzi wa hoteli ya Kichina kwa jina maarufu *Fang Wang*, unatumika kama mkakati wa kukuza na kuendeleza utawala ya Uchina katika nchi za Afrika. Viongozi wa Afrika wamemezwa na utamaduni wa kigeni hasa Kichina. Waafrika wanakula vyakula vya Kichina na hata kuvaa nguo za Kichina. Waafrika wanapata ugumu wa kukosoa na kupinga hejemonia ya Kichina hasa ikizingatiwa kwamba miradi inayoanzishwa na Uchina inawanufaisha. Uchina inatumia uwezo wake wa kiuchumi kuzindua miradi na hata kutoa mikopo kwa nchi maskini za Afrika kama njia mwafaka ya kudumisha hejemonia katika mataifa haya. Hejemonia inakua kwa haraka kwa sababu viongozi wa Afrika wanaongozwa na tamaa na ubinafsi. Ubinafsi na ulafi unawakosesha uhuru wa kutunga sera za kulinda taifa dhidi madhila ya hejemonia. Viongozi wa

Afrika wako tayari kunufaika kutokana na hejemonia inayokuzwa huku wakiwatupia wananchi wao makombo ya faida wanazopata. Nchi zilizoendelea kama vile Uchina zinatumia udhaifu wa uongozi wa Afrika kukuza na kudumisha hejemonia kwa kutumia ufadhili wa miradi anuwai. Hapa watawaliwa wanaridhia hejemonia kwa kutarajia faida na manufaa kutokana na miradi hiyo. Miradi inatumika kama chambo cha kuvuta watawaliwa karibu ili wakubaliane na matamanio ya mahejemoni.

Pia, waziri Mkurutu katika *Msimu wa Vipepeo* anaanzisha mfuko maalum wa saratani kama mchango wake kwa jamii hasa baada ya kudanganya umma kwamba mamake mzazi (Ma'kache), amefariki kutokana na saratani ya maziwa. Kulingana na waziri, hii inakuwa njia ya kumkumbuka marehemu mamake. Mfuko maalum wa saratani ni mkakati mwafaka anaoutumia waziri Mkurutu kufunika uovu wake na kuwasadikisha raia kwamba yeye ni kiongozi wa kipekee anayejali maslahi yao. Huu ni mkakati ambao wanasiasa wengi wanatumia kama njia ya kuficha uovu wao. Aghalabu watawaliwa kwa kupokea misaada na miradi inayoanzishwa na mahejemoni, wanaishia kutodadisi na kutokosoa hejemonia inayokuzwa. Kwa watawaliwa wasiojali, kilicho muhimu ni faida ambazo zitatokana na miradi inayozinduliwa. Miradi inawapofusha raia macho wasije wakaasi dhidi ya hejemonia iliopo na kuanzisha vuguvugu la mageuzi.

Msimu wa uchaguzi unapokaribia, wanasiasa katika *Msimu wa Vipepeo* wanasafiri hadi mashinani na kuzindua miradi mbalimbali. Miradi hii, aghalabu, haikamilishwi hadi msimu mwingine wa uchaguzi utakapokuja. Kwanza, waziri Mkurutu anazindua mradi wa kuchimba chemichemi kadhaa za maji. Pili, anazindua mradi wa vipepeo unaomletea sifa sufufu kote kote. Watu wote wanachangamkia mradi huu huku wakimsifu waziri. Kadhalika, Mkurutu anatumia hazina yake kujenga vituo vya polisi hususan siku za kampeni ya uchaguzi ambazo zinaambatana na ukosefu wa usalama. Huu ni mkakati ambao Mkurutu anatumia wakati wa kampeni za uchaguzi kukuza na kudumisha ushawishi wake wa kisiasa. Wanasiasa wanatafuta ridhaa kutoka kwa watawaliwa kupitia uzinduzi wa miradi ambayo kamwe haikamilishwi hasa baada ya kupigiwa kura. Mahejemoni kwa kawaida wanachezea akili za watawaliwa kwa kuwawasilisha mawazo ambayo yanawaacha katika hali ya uhitaji. Akili za raia maskini zikishajazwa tamaa ya mambo mazuri, wanasiasa hatimaye wanawasilisha mambo hayo kwa njia ya ahadi ambazo zitatimizwa tu iwapo wataridhia hejemonia. Kwa hivyo, ahadi za miradi ni mikakati ya kuwanasa raia ili waidhinishe kuwepo kwa hejemonia katika jamii. Faida na manufaa madogo yanayoahidiwa yanawapumbaza raia kiasi cha kutoona ufisadi, ukatili na unafiki inaofichika katika hejemonia. Kwa hivyo, raia wanaridhia na kuidhinisha hejemonia kwa matumaini ya kupata manufaa fulani hata kama ni madogo kutokana na miradi inayozinduliwa na mahejemoni.

Wanasiasa hutoa ahadi za ufufuzi wa magofu ya viwanda vilivyofilisika na kuporomoka kama njia moja muhimu ya kuunda nafasi za ajira hususan kwa vijana. Waziri Mkurutu katika *Msimu wa Vipepeo* ni mfano mzuri wa viongozi kama hawa.

Mkurutu anaahidi kufufua kiwanda cha sukari na kingine cha njugu za makademia. Viwanda hivi ni magofu sasa baada ya kufilisika na kuporomoka miaka mingi iliopita. Mkurutu anaahidi kuwa mipango kabambe itafanywa kuhakikisha kuwa rasilimali nzuri kama hizo hazipotei. Ahadi hizi (zisizotimizwa) zinawapa raia hususan wakulima matumaini mengi ya uhai kwa sababu maisha yao yanategemea zaraa. Ahadi za ufufuzi wa viwanda ni mkakati wa kuwafanya raia waendelee kuchangamkia uongozi uliopo na kwa njia hii kuridhia na kuidhinisha hejemonia. Lakini kabla ya kutimizwa kwa ahadi walizotoa, mahejemoni wanaibuka na miradi na ahadi zingine mpya hasa wakati wa uchaguzi kama njia ya kuwasahaulisha raia ili waridhie hejemonia. Hii ndio sababu Gramsci (1977) akadai kuwa hejemonia inawaaminisha watu kwamba uongozi na utawala wa tabaka tawala ni wa manufaa kwao. Hivyo, hejemonia inawasadikisha watu kuwa kupata furaha katika maisha ni jambo linalowezekana. Hali hii inawezeshwa na viongozi wanaowarairai watawaliwa na kuwapa ahadi za maisha mazuri ya siku za usoni (Gramsci, 1977). Kila msimu wa siasa za uchaguzi unashuhudia ahadi chungu nzima hususan kutoka kwa viongozi wa kisiasa wanaong'ang'ania kudumisha na kuimarisha hejemonia. Viongozi wa kisiasa wanatoa ahadi hizi kama njia ya kutafuta uungwaji mkono tu. Baada ya kupewa kura na kudumisha utawala wao, viongozi wanapotea kabisa na kurudi tena msimu mwingine wa uchaguzi huku wamejihami na ahadi zingine mpya.

***Warsha na Makongamano***

Serikali ya kihejemonia inaandaa warsha na makongamano kwa lengo la kuleta pamoja wadau mbalimbali wa sekta anuwai kwa nia ya kusambaza sera zake za kiutawala. Mathalani, katika *Msimu wa Vipepeo* sera ya serikali inayohitaji wakulima wa mchele wanapovuna magunia arobanne ya mchele, watumie magunia manne pekee huku yanayosalia yakipelekwa kwenye ghala la serikali ni mawazo ya kibepari. Kama njia ya kufaulisha sera hii na kuridhisha wananchi kuwa sera hiyo ni nzuri, mabwanyenye serikalini wanaunda bodi zinazohusika na usimamizi wa kilimo cha umwagiliaji maji. Bodi hizi zinajukumishwa kuandaa warsha na makongamano ya kuchunguza mbinu za kutumiwa ili kurudufu uzalishaji wa mchele. Nia kuu hapa ni kutosheleza utashi wake nchini na pia kuuza nchi za ng'ambo ili kulipatia taifa pato kubwa. Mabwenyenye serikalini wanatumia mbinu hii kama njia ya kuwashawishi watawaliwa waidhinishe sera na mawazo yao ya kiutawala. Kimsingi mawazo haya yananuia kufaidi viongozi wenyewe lakini kwa ridhaa ya raia. Maazimio ya warsha na makongamano haya yanawashawishi watawaliwa kukubali sera na mawazo ya mahejemoni kwa kuwaonyesha namna taifa zima litanufaika. Makongamano na warsha kama hizi zinawapumbaza na kuwasahaulisha raia ukweli kwamba faida na manufaa mengi yanayotokana na jasho lao yanaishia mifukoni mwa mahejemoni. Kwa misingi hii, raia wanaridhia na kuidhinisha kuwepo kwa hejemonia kutokana na ushawishi wanaopata mintarafu maazimio ya makongamano na warsha.

Katika jitihada za kuendeleza na kudumisha hejemonia, viongozi wa kisiasa wanashirikiana na mashirika ya kimataifa kufadhili makongamano ya kujadili masuala ibuka katika jamii. Katika *Msimu wa Vipepeo,* mashirika ya nchi za kigeni kama vile shirika la GTZ la Ujerumani linadhamini kongamano la kujadili mikakati ya kupambana na tatizo la ukame ili wakulima waendelee kupata mavuno mengi. Hata hivyo, asilimia tisini ya mapato ya mavuno yenyewe yanaishia mifukoni mwa viongozi wachache walafi walioko serikalini. Kwa mujibu wa mzee Kitali, mmoja wa wakulima katika eneo la Mwetare, eneo zima la Mwetare halina huduma za kimsingi kama vile umeme, hosipitali na shule nzuri ilhali raia wanamenyeka kwa kazi ngumu huku wanaofaidi ni wengine (uk 17). Warsha na makongamano kwa hivyo yanatumika kuwapumbaza wakulima wasione umuhimu wa kula jasho lao. Warsha na makongamano haya yanapangwa kwa werevu na mahejemoni kama njia mwafaka ya kuwapumbaza watawaliwa ili wasikosoe wala kupinga hejemonia inayokuzwa. Kupitia makongamano haya, raia wanasadikishwa kuwa utawala uliopo unajali maslahi yao. Raia wanafumbwa macho na shughuli za makongamano wasione ukweli kwamba mahejemoni ndio wanafaidika pakubwa kutokana na jasho lao.

Warsha na makongamano yanaandaliwa na kisha kutafutiwa ufadhili kutoka kwa mataifa yalioendelea. Fabio Mkalla, Mwanasheria Mkuu wa serikali katika *Msimu wa Vipepeo* anasema: ".... kuna warsha ya mikakati ya kuimarisha utalii... tunanuia kuwa na warsha kama sita hivi! Tumepewa udhamini na Ujerumani, Uholanzi na Uingereza kufanya hivi na lazima hela hizi zitumiwe yahe!" (uk 147). Warsha zinaandaliwa kuwasadikisha raia kuwa viongozi serikalini wanafanya kazi ilhali ukweli ni kwamba viongozi hawa wanatumia fursa hizi kujitajirisha na kujinufaisha kwa kupata pato la ziada kupitia marupurupu na njia zingine za kifisadi. Viongozi wanaandaa makongamano na warsha za kuweka mikakati ya kuboresha sekta anuwai katika jamii. Nia ya makongamano haya hata hivyo ni kuwanufaisha mahejemoni wanaoyaandaa bali sio kunufaisha umma. Makongamano ni kama mrija wa kunyonya rasilimali ya umma huku raia wakipumbazwa kwa mawazo na sera za kuleta maendeleo kwa jamii nzima. Hatimaye, mataifa ya kigeni yanayofadhili makongamano na warsha katika mataifa yanayoendelea pia yanatumia njia hii kukuza na kudumisha hejemonia katika mataifa fadhiliwa. Aghalabu viongozi wa mataifa fadhiliwa wanaridhia matakwa ya wafadhili ili kuendelea kunufaika kupitia makongamano na warsha zinazofadhiliwa. Kwa hivyo, tamaa, ulafi na ubinafsi wa viongozi ni sababu moja kubwa ya kuridhia na kuidhinisha hejemonia inayokuzwa na kuendelezwa kwa njia ya makongamano na warsha zinazofadhiliwa na mataifa yalioendelea.

### *Uchochezi na Maandamano*

Upinzani na ukosoaji wa hejemonia ukianza kujitokeza katika jamii, viongozi wanakabiliana na hali hii kwa kutumia mbinu ya uchochezi wa raia. Viongozi wa kisiasa wanachochea raia (wafuasi wao) kuandamana huku wamebeba mabango na kuimba nyimbo za kuwatetea viongozi wao. Mathalani, Waziri Mkurutu katika

*Msimu wa Vipepeo* anapanga njama na kuwashawishi wanaeneobunge lake kuandamana kwa nia ya kutetea utendakazi wake. Akiwachochea raia wa eneo bunge lake anasema: "Hawa hawanifuati mimi kama Jay Mkurutu. La. Wanachotaka ni kulitundika msalabani kabila letu lote! Hii ni njama ya watu wanaotuonea gere kwa maendeleo yetu,'' (uk 208). Wanaeneobunge lake wanaandamana huku wamebeba mabango kuwalaumu wapinzani wa hejemonia inayokuzwa na waziri. Mahejemoni wanachochea raia wawaunge mkono dhidi ya wapinzani na wakosoaji wao. Watawaliwa kwa kuridhia mawazo ya viongozi wao, wako tayari kutangazia ulimwengu jinsi viongozi wao walivyo na moyo mzuri na kwamba hawezi kuhusika katika kashfa zozote za uhalifu. Viongozi wanapokabiliwa na upinzani unaokosoa utawala wao wanaishia kuchochea raia hasa watu wa kabila lao dhidi ya makabila mengine. Hili linafanywa kwa werevu, ujanja na hila ili kupanda mbegu za chuki kwa kuwafitinisha watu wa kabila analotoka kiongozi na makabila wanayotoka wapinzani na wakosoaji wa hejemonia. Aghalabu hali hii inazua uhasama na vita vya kikabila katika jamii. Makabila ya nchi moja yanapigana yenyewe kwa yenyewe huku wanasiasa wakitafuta njia ya kukomesha vita hivyo. Hatimaye, mahejemoni wale wale wanaochochea vita vya kikabila wanakuwa msitari wa mbele kutafuta maridhiano na amani kati ya makabila yanayozozana na kupigana. Hii ni njia ya kuwashawishi tena watawaliwa waridhie na kuidhinisha mahejemoni kuendeleza utawala wao. Raia wanafumbia macho uovu wa viongozi wao na kuishia kuridhika na hejemonia inayoendelezwa kwa uchochezi wa kabila moja dhidi ya kabila lingine.

### *Mabadiliko katika Baraza la Mawaziri*

Mabadiliko katika baraza la mawaziri ni miongoni mwa mbinu ambazo Rais Kamaliza Rungu-ya-Kioga ametumia kukuza na kudumisha hejemonia katika *Msimu wa Vipepeo*. Rais anapotambua manung'uniko miongoni mwa raia kuhusiana na utawala wake, kwa werevu na hadaa anafanya mabadiliko katika baraza la mawaziri kama njia ya kutuliza joto la uasi miongoni mwa raia. Mabadiliko katika baraza la mawaziri yanajumuisha kuhamisha baadhi ya mawaziri kutoka wizara moja hadi nyingine na wengine kufutwa kazi. Kwanza, mawaziri ambao ni wafuasi sugu wa rais japo wana kashfa nyingi za ufisadi na uhalifu wanahamishiwa wizara mpya. Mathalani, waziri Mkurutu anahamishwa kutoka Wizara ya Utalii hadi Wizara ya Afya huku waziri Ngao akichukua hatamu za uwaziri katika Wizara ya Utalii na Mazingira. Pili, mawaziri wasiokubaliana na Rais kwa baadhi ya mambo wanafutwa kazi. Mathalan, waziri Fumo ambaye ni mchapakazi, mtetezi wa haki za wakulima na waziri wa pekee anayejitokeza kupinga baadhi ya mapendekezo ya wafadhili wakuu wa nchi kuhusu mabadiliko katika sekta ya zaraa, anafutwa kazi. Rais anahakikisha kuwa utawala wake unadumu na kuimarika kwa kuwanyamazisha wakosoaji wa sera za uongozi. Wafanyakazi wa serikali wanaotetea ukuaji wa uchumi wa nchi kwa faida ya raia wa nchi husika wanatupwa mbali kwa kufutwa kazi. Kuhamisha mawaziri pamoja

na kufuta wengine kazi ni mkakati unaotumiwa na mahejemoni kuwashawishi raia waridhike na utawala uliopo. Aidha, mbinu hii inawatia woga wafanyakazi wote wa umma ili kwamba wasijaribu kukosoa hejemonia inayokuzwa la sivyo wamwage unga. Raia wanaaminishwa na kuridhishwa kuwa hejemonia iliopo inajali maslahi ya umma na kwa hivyo inafaa kuungwa mkono. Mwandishi wa *Msimu wa Vipepeo* anasema:

> Rais Kamaliza Rungu-ya-Kioga, kiongozi wa nchi, baba-na-mama kwa wafuasi wake wa karibu, alifanya mabadiliko katika baraza lake la mawaziri. Taarifa iliyotoka ikulu ya rais, iliyotangaza mabadiliko yenyewe, ilisema kuwa yalikuwa yamenuiwa kuuimarisha utendakazi wa serikali. Kwamba yalionyesha mwelekeo imara wa serikali na kusisitiza nia ya serikali kuendelea kuutumikia umma kama walivyoapa viongozi wakati wanautwaa uongozi' (uk 153).

Rais anafanya mabadiliko ya uongozi wake kama njia ya kuwafumba raia macho. Anafanya mabadiliko ya kuwahadaa raia kwamba utendakazi na utoaji wa huduma kwao utaboreshwa. Hata hivyo, wafanyakazi wa umma wanaofutwa kazi bila ya kutarajia kwa sababu za kukosoa mahejemoni wanaachwa katika hali ya kusikitisha. Hali hii inawafanya baadhi ya watu waoga kujiapia kimoyomoyo kuwa hawatafanya kosa la kuikosoa wala kupinga hejemonia. Kwa njia hii, mahejemoni wanafaulu katika lengo lao la kuwatia watu uwoga ili wasije wakakosoa hejemonia. Hali hii inashadidia mawazo ya Nella (2017) anapodai kuwa siku hizi hejemonia haihusu tu matumizi ya nguvu katika uongozi bali kwa kiwango kikubwa hutegemea ushawishi wa watu wengi kwa kuwapendekezea na kuwawasilishia hali na mambo kwa njia ambayo ni vigumu sana kuyapinga au kuyakataa. Idadi kubwa ya raia kwa hofu na uwoga wanaridhia na kuidhinisha kuendelea kwa hali jinsi ilivyo. Hejemonia inakua na kuendelea kunawiri katika mazingira kama haya yenye rutuba inayotokana na uwoga wa raia wasio tayari kupoteza kazi zao; kazi ambazo zinawasaidia kujikimu kimaisha.

## Hitimisho

Katika makala haya, inabainika wazi kuwa katika *Msururu wa Usaliti, Majilio ya Mkombozi, Dharau ya Ini* na *Msimu wa Vipepeo,* viongozi wanafanikiwa kukuza na kuendeleza hejemonia katika siasa na uchumi kwa kutumia mikakati chungu nzima. Mikakati iliyotumiwa ililenga kuwapumbaza na kuwashawishi watawaliwa ili waridhie na kuidhinisha hejemonia pasina kukosoa mawazo yaliyokuzwa na viongozi. Hata hivyo, mikakati hii ilifaulu tu pale ambapo raia wenyewe waliridhia na kuidhinisha uwepo wa hejemonia katika jamii. Mawazo haya yamepigwa jeki na maoni ya Fontana (2008) na Gramsci (1978) waliyoshikilia kuwa ushirikiano, mwafaka na makubaliano kati ya watawala na watawaliwa ni msingi wa kunawiri na kufaulu kwa hejemonia katika jamii. Kwa hivyo, kuwepo kwa hejemonia katika jamii kunatokana na ridhaa na idhini ya raia wanaotawaliwa.

## Marejeleo

Artz, L. & Murphy, B. O. (2000). *Cultural Hegemony in the United States*. California: Sage Publications.

Bates, T. R. (1975). *Gramsci and the Theory of Hejemony*. Journal of the History of Ideas. Vol 36, No. 2 (April, 975), pp. 351-366. University of Pennsylvania Press. Ilitembelewa 13/09/ 2018, 11:55 mchana. https://www.jstor.org/stable/2708933.

Boggs, C. (1976). *Gramsci's Marxism*, Pluto Press Limited, London.

Femia, J. (1975). 'Hegemony and Consciousness in the Thought of Antonio Gramsci', *Political Studies*, vol. 23, no. 1, pp. 29 - 48

Fineman, M. (2001). "Dependencies", In N. Hirschman and U. Liebert (eds) Women and Welfare: Theory and Practice in the United States and Eorope. New Brunswick NJ: Rutgers University Press.

Fontana, B. (1993). *Hegemony and Power: On the Relationship between Gramsci and Machiavelli*. London: University of Minnesota Press.

Fontana, B. (2008). 'Hegemony and Power in Gramsci'. In Howson, R. and Smith, K. (eds), *Hegemony: Studies in Consensus and Coercion*. Routledge: New York

Forgacs, D. (1988). *An Antonio Gramsci Reader: Selected Writings 1916-1935*. London: Schonken Books.

Gerratana, V. (1975). *Antonio Gramsci, Quarderni del Carcere* vols 1-4. Einudi, Turin.

Gramsci, A. (1995). *Further selections from the prison Notebooks*. Edited and translated by Derek Boothman. Minneapolis: University of Minnesota Press.

Gramsci, A. (1978). *Selections from the Political writings 1921-1926*. London: Lawrence and Wishart.

Ives, P. (2004). *Language and Hegemony in Gramsci*. London: Pluto Press.

Lautzes, S. na Hammock, J. (1996). *Coping with Crisis: Coping with Aid*. Medford: MA: Feinstein International Famine Center, Tufts University.

Lenin, V. (2004). *The State and Revolution*. Montana: Kessinger Publishing.

Lensink, R. na White, H. (1999). *Aid Dependence: Issues and Indicators*. Expert Group on Development Issues.

Mbatiah, M. (2010). *Msururu wa Usaliti*. Nairobi. East African Educational Publishers Limited.

Mbatiah, M. (2016). *Majilio ya Mkombozi*. Nairobi: Moran (E. A) Publishers Limited.

Ransome, P. (1992). *Antonio Gramsci: A New Introduction*. London: Harvestor Wheatsheaf.

Strinati, D. (1995). *An Introduction to the Theories of Popular Culture*. London: Routledge.

Wamitila, W. K. (2007). *Dharau ya Ini*. Nairobi: Vide-Muwa Publishers Limited.

Wamitila, W. K. (2006). *Msimu wa Vipepeo*. Nairobi. Vide-Muwa Publishers Limited.